


JINSI YA KUPATA USAIDIZI

- Piga simu kwa nambari yetu ya huduma ya kisheria, inayosimamiwa na mshirika wetu, Huduma za Kisheria za Vermont (*Legal Services Vermont*), namba ni: 1-800-889-2047
- Kwa taarifa zaidi kuhusu mradi wa mchunguzi maalum wa utunzaji wa muda mrefu tembelea tovuti yetu: <https://www.vtlegalaid.org/vermont-long-term-care-ombudsman-project>

Burlington | Montpelier | Rutland

Springfield | St. Johnsbury



UNAHITAJI MKALIMANI?

Pata usaidizi kutoka kwetu
kwa lugha yako.

Piga simu nambari
1-800-889-2047.

Tuambie jina na nambari
yako ya simu.
Sema Kiswahili.



**VERMONT
LEGAL
AID**
USAIDIZI WA KISHERIA
WA VERMONT

KUSHIRIKIANA KWA AJILI YA HAKI



MRADI WA MCHUNGUZI MAALUM WA UTUNZAJI WA MUDA MREFU

Msaada wa bila malipo kwa wakaazi wa Vermont wanaopokea huduma ya utunzaji wa muda mrefu katika makao ya kuwatunzia wagonjwa, makao ya huduma ya utunzaji, makao ya wanaohitaji usaidizi wa kila siku, na katika jamii kupitia mpango wa Choices for Care.

SWAHILI

<https://vtlawhelp.org>

| 1-800-889-2047



SISI NI AKINA NANI

Vermont Legal Aid (Usaidizi wa Kisheria wa Vermont) ni kamuni ya sheria ya jimbo nzima, isiyo ya faida yenye misheni ya haki za kijamii. Tunatoa huduma za kisheria bila malipo kwa wakaazi wa Vermont wenye matatizo ya kisheria yanayotishia haki na ustawi wao.

Mradi wa **Mchunguzi maalum wa Huduma ya Utunzaji** unakuza haki za wakaazi wa Vermont wanaopokea huduma za utunzaji wa muda mrefu. Pia tunapigania mabadiliko yanayosababisha utunzaji bora na maisha bora.

"Nilivunjika moyo kwa sababu binti wangu anaishi nichini Kanada. Mwana wangu anaishi Florida. Hakuna mtu wa kunisaidia. Nina umri wa miaka 83. Sikujua cha kufanya... Nilisikia kuhusu mpango wa Mchunguzi maalum wa Usaidizi wa Kisheria. Ni jambo bora zaidi ambalo limeshawahi kunitendekea"

- **Mteja wa VOP**

JINSI TUNAVYOSAIDIA

Kuchunguza Lalamiko

Tunatambua, tunachunguza, na tunatatua malalamiko ya au kuhusu watu wanaopokea huduma za utunzaji za muda mrefu.

Kujitetea

Tunawasaidia watu wapaze sauti zao kuhusu utunzaji wao.

Huduma na Utunzaji Unaozingatia Jamii

Tunawasaidia watu walio katika Mpango wa Choices for Care kupokea huduma za utunzaji wa muda mrefu katika jamii.

Shughuli za Mpango

Tunatembelea vituo vya utunzaji wa muda mrefu ili tuzungumze na wakaazi na tufuatilie hali, tunaelimisha watoaji huduma kuhusu haki za wakaazi, na tunatoa taarifa kwa umma kuhusu huduma za utunzaji wa muda mrefu na machaguo.

Utetezi wa Mifumo

Tunasaidia katika kutambua nyanja zenyе matatizo katika mfumo wa utunzaji wa muda mrefu na kisha tunapigania uboreshaji.

Utetezi wa Sera

Tunapigania sheria na sera za kuboresha huduma ya utunzaji na ubora wa maisha ya wakaazi wa Vermont wanaopokea huduma ya utunzaji wa muda mrefu kwenvye mazingira ya kituo na katika jamii kuitia mpango wa Choices for Care.

WATU TUNAOWASADIA

Tunafanya kazi na watu wanaopokea huduma za utunzaji wa muda mrefu katika:

- Makao ya kuwatunzia wagonjwa
- Makao ya huduma ya utunzaji
- Makao ya wanaohitaji usaidizi wa kila siku
- Makao ya kuwatunzia watu wazima
- Jamii kuitia mpango wa Choices for Care



**VERMONT
LEGAL
AID**

Mradi wa Mchunguzi maalum wa Huduma ya Utunzaji wa Muda mrefu